

HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA



TAHADHARI DHIDI YA UGONJWA WA EBOLA

MKURUGENZI WA MJI TUNDUMA ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUWA MLIPUKO WA UGONJWA WA EBOLA UMETOKEA KATIKA NCHI JIRANI YA KONGO.

UGONJWA HUU HUAMBUKIZWA KUTOKA KWA MNYAMA KWENDA KWA BINADAMU AU BINADAMU KWENDA KWA BINADAMU KWA NJIA YA HARAKA KWA KULA AU KUGUSA VIUNGO NA MAJIMAJI YA WANYAMAPORI KAMA VILE POPO, NYANI, KIMA NA SOKWE WENYE MAAMBUKIZI YA UGONJWA HUO.

PIA UGONJWA HUU HUENEA KUTOKA KWA MTU MMOJA HADI MWINGINE KWA NJIA YA KUGUSA MAJIMAJI YA MWILI KAMA VILE DAMU, MATAPISHI, JASHO, MATE, MACHOZI, MKOJO AU KINYESI KUTOKA KWA MTU ALIYEKWISHAAMBUKIZWA. PIA KUGUSA MAITI YA ALIYEAMBUKIZWA AU KUGUSA VYOMBO NA NGUO ZILIZOTUMIWA NA MTU ALIYEAMBUKIZWA HUSABABISHA MAAMBUKIZI YA UGONJWA HUU.

DALILI ZA EBOLA NI PAMOJA NA KUWA NA HOMA KALI YA GHAFLA, KULEGEA KWA MWILI, MAUMIVU YA MISULI, KUUMWA KICHWA NA VIDONDA KOONI, KISHA KUFUATIWA NA KUHARA, KUTAPIKA, NA VIPELE.

BAADHI YA WAGONJWA HUTOKWA NA DAMU SEHEMU ZA WAZI ZA MWILI KAMA VILE MACHONI, PUANI, MASIKIONI, MDOMONI, NA NJIA YA HAJA NDOGO NA KUBWA.

UGONJWA WA EBOLA HAUNA MATIBABU MAALUM WALA CHANJO, BALI MGNJWA HUTIBIWA KUTOKANA NA DALILI ZITAKAZOAMBATANA NA UGONJWA HUO.

UGONJWA HUU UNaweza KUZUILIKA KWA KUEPUKA KUGUSA AU KUNGIWA NA DAMU, MATAPISHI, KAMASI, MKOJO, MATE, MACHOZI, KINYESI NA MAJIMAJI MENGINE YANAYOTOKA MWILINI MWA MTU MWENYE DALILI ZA EBOLA.

EPUKA KUOSHA AU KUGUSA MAITI YA MTU ALIYEKUFA AKIWA NA DALILI ZA EBOLA, BADALA YAKE TOA TAARIFA KWENYE KITUO CHA HUDUMA ZA AFYA KWA USHAURI

TANGAZO HILI LIMETOLEWA TAREHE 22 MEI 2018 NA

Ndugu Kastori G. Msigala
**KAIMU MKURUGENZI WA MJI
HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA**